**MUHTASARI WA MWONGOZO WA MAKUNDI YA WATU WALIO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI MRADI.**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, imeandaa mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari nchini utakaofahamika kwa kifupi kama SEQUIP. Madhumuni ya mradi huu ni kuongeza ufikiwaji wa elimu ya sekondari, kuwapatia wasichana mazingira bora ya kujifunza na kuboresha uhitimu bora wa elimu ya sekondari kwa wasichana na wavulana

**Eneo la kwanza (1):** Kuwajengea Wasichana Uwezo Kupitia Elimu ya Sekondari na Stadi za Maisha.

1.1 Kuanzisha shule salama: Utekelezwaji wa shule salama unahusisha: (i) kutoa mafunzao uongozaji wa shule na ushauri kwa walimu; (ii) mafunzo ya stadi za maisha kwa wanafunzi; (iii) huduma za mafunzo ya kanuni za mwenendo na jinsia kwa kutumia mbinu za pedagogical; (iv) kuwajengea walimu wakuu, bodi za shule kuhusu ukatili wa kijinsia na masuala ya shule salama; (v) Kuwepo na mfumo wa ufuatiliaji mashuleni na madarasani kwa ajili ya utambuzi wa awali na kuingilia kati wasichana wali katika hatari ya kuacha shule; na (vi) mfumo wa kijamii kwa ajili ya usalama mashuleni.

1.2 Kukuza uhitimisha wa elimu ya sekondari kwa wasichana kupitia njia mbadala za ubora wa elimu, ikiwa pamoja na:

- Kuwepo na mpangilio wa mfumo wa TEHAMA kwa ajili ya kufuatilia uachaji shule kwa wasichana katika ngazi ya taifa na wilaya na kutoa taarifa muhimu kwenye mpango na utekelezaji wa njia mbadala za ubora wa elimu (AEP)
- vituo vya njia mbadala za elimu na mamlaka ya serikali za mitaa (LGAs) watafanya shughuli za ufikiwaji wa wasichana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu kwenye jamii ikiwa pamoja na shughuli za kufanyika kwa mikutano ya kijamii ya njia mbadala za elimu, kutoa taarifa kupitia redio na televisheni, mabango na vipeperushi.
- kukuza ufikiwaji wa njia mbadala za ubora wa elimu kupitia (i) upanuzi wa mtadao wa vituo njia mbadala za ubora wa elimu; na (ii) kutoa punguzo la ada kwa wasichana wanaoishi katika mazingira magumu
- Ubora wa kifurushi cha uimarishaji wa wanafunzi kujifunza njia mbadala za ubora wa elimu pia zitatekelezwa.

**Eneo la Pili (2):** Kufundisha na Kujifunza kwa Ufanishi kwa Kuwezesha Mifumo ya Kidigitali

2.1 Ufanisi katika kufundisha na kujifunza

- kifurushi kidogo ambacho kitakuwa na rasilimali muhumu za kufundushia na kujifunza kwenye shule zote: kifurushi hicho kitakuwa na vitabu vya kutosha na muongozo wa mwalimu kwenye masomo muhimu (Kiingereza, Hisabati na Sayansi)
- Usawa, walimu kwa kuzingatia usawa wa kijinsia watapelekwa mashuleni
- uendeleaji wa huduma za mafunzo kwa walimu wa sekondari kwenye masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi kwa ajili ya kuboresha mafunzo ya darasani kwa vitendo.
- kutathmini ujifunzaji wa wanafunzi wa elimu ya sekondari ili kutoa nafari ya kurekebisha: kukubali uingiliaji kai wa awali ili kuzuia wanafunzi wa kike kuacha shule kwa ajili ya tatizo la uelewa/kijifunza.

2.2 Kuwezesha mfumo wa kidigitali wa kufundishia masomomo ya hisabati, sayansi and kiingereza

- Kuanzisha mfumo wa TEHAMA kwenye mpango na mkakati wa elimu kwa elimu ya sekondari
- yaliyomo kwenye mfumo wa kidigitali yaunganishwe na fungu la kufundishia masomo ya kiingereza. hisabati na sayansi.

**Eneo la tatu (3):** Kupunguza Vikwazo vya Elimu kwa Wasichana Kupitia Uwezeshaji wa Upatikanaji wa Elimu ya Sekondari

- Kupanua mtandao wa elimu ya sekondari ili kupunguza umbali wa shule za sekondari hasa vijijini. SEQUIP itatoa ufadhili kupitia maradi kwa kuangalia idadi ya namba za shule kwenye kila mamlaka ya serikali za mitaa ili kufikia kiwango cha chini cha miundombinu.
- kutoa msaada ili kuinua shule za sekondari zilizopo kwa kutumia kiwango cha chini cha fungu la miundombinu (idadi ya madarasa/wanafunzi, utoshelezaji wa maji na vifaa vya usafi wa mazingira, maabara za sayansi, umeme n.k.). Lengo ni angalau asilimia 50 ya shule zote zilizopo kwenye mamlaka zote za serikali za mitaa zitaweza kufikia malengo ya chini yaliyowekwa,

**Eneo la Nne (4):** Kutoa Msaada wa kitaalamu, Kufanya Tathmini ya Athari ya Mradi na Uratibu wake.

**Muktadha wa Mwongozo wa Makundi ya Watu Walio kwenye Mazingira hatarishi**

Mwongozo huu wa Makundi ya Watu Walio katika Mazingira Hatarishi umeandaliwa kwa kufuata vipengele muhimu vya sheria za Tanzania, na Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii wa Benki ya Dunia. Vigezo tisa vilivyoainishwa kwatika Mwongozo wa Masuala ya Mazingira na Kijamii wa Benki ya Dunia vimetumika katika kuandaa Mwongozo huu wa Makundi ya Watu Walio kwenye Mazingira hatarishi. Kigezo Na. 7 kinachohusu Jamii zinazoishi kijadi zilizokuwa hazipewi kipaumbele kihistoria katika utoaji wa huduma kutokana na mifumo yao ya maisha zinazopatikana Kusini mwa Jangwa la Sahara ambacho kinataka miradi kuongeza nafasi kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kushiriki na kunufaika na shughuli za maendeleo katika hali ambayo haihatarishi ustawi wao, pamoja na mila na tamaduni zao. Mwongozo unaelekeza namna ya kushirikisha kikamilifu, makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi, katika kuandaa na kutekeleza mradi huu wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari katika ngazi ya jamii.

Kulingana na Kigezo Na. 7, kwa mazingira ya Tanzania, makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi ni pamoja na wawindaji na wakusanyaji wa matunda, wafugaji na jamii zinazofanya kilimo na ufugaji (ambazo ni Wahadzabe, Waakie, Wasandawe, Wamasai, na Wabarbaigi). Makundi haya yanapatikana kwa wingi maeneo ya Kaskazini mwa Tanzania.

**Athari na Udhibiti wake**

Katika muktadha wa Mradi, makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi yanaweza kunufaika kupitia:

i. Kuongezeka kwa nafasi za wanafunzi wanaojiunga na kuhitimu masomo kutokana na kuongezeka kwa idadi ya shule au vyumba vya madarasa, ubora wa mazingira ya kujifunzia pamoja na walimu wa kutosha ambavyo huchangia kuongeza ubora wa elimu. Aidha, mpango wa kutetea baadhi ya makundi, mipango ya misaada ya kijamii, huduma za ushauri kwa wanafunzi vitaongeza motisha ya wanafunzi kuhudhuria shule mara kwa mara na kuhitimu elimu ya sekondari.
ii. Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya sekondari ya juu kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia kwa kujenga vyumba vya madarasa, maabara, miundombinu ya usafi na huduma za maji.
iii. Matokeo chanya yatokanayo na mafunzo bora katika masomo ya Hisabati, Kiingereza na sayansi kwa wanafunzi wanaotoka kwenye makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kupitia upatikanaji wa vitabu vya kutosha vya masomo hayo.
iv. Uhamasishaji unaolenga kupunguza imani potofu kuhusu elimu kwa baadhi ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.
v. Kupunguza ndoa na mimba za utotoni kwa kuwapa wanafunzi ushauri na elimu ya stadi za maisha.

Athari kuu kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishini zimeainishwa katika jedwali sambamba na hatua zinazohitajika kuchukuliwa ili kupunguza hatari na athari hizo. Wakati wa kuandaa mwongozo wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi, na kama itahitajika, tathmini nyingine zitajumuishwa ili kutatua athari maalum zinzohusiana na eneo la mradi.

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ufikiwaji wa shule/ Vifaa vya Njia Mbadala za Ubora wa Elimu | Kutokuwepo na usawa/ njia mbadala za ubora wa elimu kutokana na umbali kutoka kwenye jamii, hususani kama shule ipo/ inapojengwa karibu na kijiji chenye wakazi wengi au sehemu yenye wakazi ambao hawatoki kwenye makundi ya watu walio katika mazingira hatarishini. | • Kuitia mipango ya Mamlaka za Serikali za Mitaa inayohusiana na shule yanatakiwa kuzingatia mahitaji ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.<br>• Kuanzishwa kwa nafasi mbadala, kama vile kuwahamishia wanafunzi wanaotoka jamii zilizoko katika mazingira hatarishi kwenye shule za bweni.<br>• Maeneo ya makazi ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi yanahitaji kuzingatiwa wakati wa kupanga maeneo ambayo miradi ya ujenzi na ukarabati itaanzishwa.<br>• Kuwashirikisha makundi ya watu walio katika mazingira hatarishini kuhusu upatikanaji wa elimu ya sekondari ili kukidhi mahitaji yao. | Maandalizi ya Mradi | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| 2. | Kuchangia katika maendeleo ya | Kutokukubalika, au kupata ushirikiano hafifu kutoka kwenye makundi ya watu walio | • Kuhimiza ushiriki wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kwenye mipango, | Endelevu lakini inasisitizwa | Timu ya Uratibu wa Mradi, |

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | shughuli za mradi | katika mazingira hatarishi kutokana na kutohusishwa kikamilifu kuanzia hatua za awali za mradi. Hii ni pamoja na kuzingatia aina ya shule inayojengwa, mfano shule ya bweni au daharia na pia mapendekezo kwenye vipengele kama program za shule salama. | utekelezaji na usimamizi wa miradi kwa kutumia Mwongozo wa Ushirikishwaji Wadau.<br>• Kushirikisha kikamilifu wawakilishi wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi katika ujenzi wa shule pale inapohitajika.<br>• Ushirikishwaji wa wadau kwa kutumia lugha wanayoielewa na kwa namna ambayo inakidhi mila na desturi zao. | kufanyika wakati wa maandalizi ya mradi | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| 3. | Upatikanaji wa rasilimali za asili | Migogoro inaweza kutokea kutokana na matumizi ya rasilimali za asili zitakazohitajika kwa ajili ya ujenzi na uendeshaji wa shule, hususani rasilimali za maji na maeneo ya machimbo ya mchanga na kokoto kwa ajili ya ujenzi, n.k. Mgogoro juu yamatumizi ya rasilimali za maji ni jambo linaloweza kutokea katika maeneo yaliyokumbwa na ukame au kuathirika na mabadiliko ya tabia nchi. | • Ushirikiswaji kuhusu matumizi ya rasilimali zilizoainishwa.<br>• Makubaliano kuhusu matumizi ya pamoja ya rasilimali.<br>• Mashauriano na makubaliano yafanyike kuhusu maeneo ya kuchimba mashimo ya mchanga kwa ajili ya ujenzi na ufukiaji wa mashimo hayo baada ya mradi kuisha.<br>• Kama itahitajika, rasilimali mbadala ziainishwe bila kujali umbali na upatikanaji wake. | Endelevu lakini inasisitizwa kufanyika wakati wa maandalizi ya mradi | Mamlaka za Serikali za Mitaa<br><br>Kamati ya Ujenzi wa Shule |

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| 4. | Uhamiaji | Uwepo wa shule ya sekondari unaweza kuchangia uhamiaji wa watu ambao unaweza kuibua migogoro ya ardhi, matumizi ya rasilimali za asili na fursa zisizo sawa zitokanazo na ujenzi wa shule | • Mabaraza ya vijiji/Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuzingatia athari zinazoweza kutokea wakati wa kuandaa eneo la mradi.<br>• Kujenga uelewa kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi<br>• Utekelezaji wa Sheria ya Ardhi na kanuni zake | Endelevu lakini inasisitizwa kufanyika wakati wa maandalizi ya mradi | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| 5. | Uchaguzi wa maeneo ya ujenzi wa miundombinu | Kuvamiwa kwa ardhi ya kijadi au maeneo ya kimila ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi ambayo husababisha uchelewaji wa mradi, migogoro, n.k. | • Kutambua uwepo wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi wakati wa mchakato wa tathmini.<br>• Ushirikishwaji wa mapema wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi ili kubainisha changamoto zilizopo pamoja na mahitaji yao ili kujua kama eneo lililochaguliwa linafaa.<br>• Kuandaa mwongozo wa ushiriki wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi,<br>• Kuanda na kuwasainisha kwa hiari fomu ya kuridhia uwepo wa | Wakati wa uendelezaji wa mradi | Mamlaka za Serikali za Mitaa<br>Kamati ya Ujenzi wa Shule |

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | mradi ili kudhibitisha kukubalika kwa mradi katika eneo husika. | | |
| 6. | Kupotea kwa mila na tamaduni | • Makundi ya Watu Walio katika Mazingira hatarishi yanaweza kuwa na hofu ya kupotea kwa mila na tamaduni zao kwa kuwapeleka watoto wao kwenye shule za sekondari ambazo hawakushirikishwa wakati wa kuzianzisha au ambazo zina watoto kutoka kwenye jamii nyingine. | • kutoa mafunzo yanayohitajika na taarifa sahihi za mila na tamaduni pamoja na umuhimu wa elimu kwa kutumia lugha za asili na watu wanaokubalika katika maeneo yao. | Kabla ya ufanyikaji eneo ( components) la mradi kwenye wilaya ambapo makundi hatarishi wanaishi<br><br>Endelevu | Timu ya Uratibu wa Mradi<br><br>Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| 7. | Ongezeko la ukatili na unyanyasaji wa kijisinsia | • Kuwepo kwa wafanyakazi wa kiume kutoka katika jamii nyingine wakati wa ujenzi wa shule, kunaweza kupelekea ongezeko la matukio ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia na maambukizi ya | • Kutoa elimu sahihi ya mila na tamaduni kwa kutumia lugha za asili na jumuishi na kampeni za kitaifa zinazofanywa kwa Kiswahili.<br>• Kuhakikisha kwamba taratibu za kupokea na kushughulikia | Kabla ya ufanyikaji eneo ( components) la mradi kwenye wilaya | Mamlaka za Serikali za Mitaa |

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | magonjwa. Aidha, tamaduni za makundi haya zinaweza kuchangia ugumu wa utoaji wa taarifa za ukatili au unyanyasaji wa kijinsia pamoja na uwepo wa baadhi ya magonjwa | malalamiko zinaruhusu makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kutoa taarifa kwa siri na kupata huduma zaidi katika ngazi za juu.<br>• Kuwepo kwa mwongozo wa maadili ya wafanyakazi ili kuepuka matokeo hasi.<br>• Kuwapa wafanyakazi mafunzo kuhusu maadili ya kazi. | ambapo makundi hatarishi wanaishi<br><br>Endelevu | |
| 8. | Kutokuzingatiwa kwa mahitaji ya wanawake na watoto kutokana na kutokuwepo kwa majadiliano ya masuala ya kijamii na kimaendeleo | • Ushiriki duni wa wanawake katika maamuzi na hivyo kusababisha shule zinazoanzishwa kutokubalika au kukubalika kwa kiasi kidogo | • Mamlaka za Serikali za Mitaa na viongozi katika jamii kuhakikisha ushirikishwaji wa wanawake kwenye majadiliano na utoaji wa maamuzi. Hii inaweza kuhitaji majadiliano ya makundi kwa wanawake kutoka kwenye makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kupitia wawezeshaji ambao wanawake hao watakua huru kujadiliana nao kwa kutumia lugha za asili.<br>• Mafunzo endelevu ya kujenga uelewa wa haki za wanawake | Kabla ya ufanyikaji eneo ( components) la mradi kwenye wilaya ambapo makundi hatarishi wanaishi<br><br>Endelevu | Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mabaraza ya Vijiji, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Asasi za Kijamii |

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kumiliki ardhi, rasilimali na kuwezeshwa kumudu maisha. | | |
| 9. | Kuongezeka kwa hali ya kushindwa kushirikishwa ipasavyo kwa Makundi ya Watu Walio katika Mazingira hatarishi kwa sababu ya changamoto za mawasiliano | Kutoshirikishwa kwa makundi ya watu walio mazingira hatarishi, jambo linalosababisha makundi hayo kutonufaika na mradi na kuathirika zaidi kuliko jamii nyingine. | • Kutumia njia za mawasiliano ambazo zitahakikisha ushiriki wa Makundi ya Watu Walio katika Mazingira hatarishi ikiwa ni pamoja na kufanya nao mikutano na kuzungumza na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotetea haki zao.<br>• Kuwashirikisha ipasavyo viongozi wa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.<br>• Kuandaa na kutekeleza mipango kazi ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kwa kila mradi.<br>• Mwongozo wa mawasiliano rasmi kwa ajili ya mradi ili kuhakikisha kuwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi yanasikilizwa, changamoto zinapatiwa ufumbuzi na malalamiko yanasikilizwa. | Kabla ya ufanyikaji eneo (components) la mradi kwenye wilaya ambapo makundi hatarishi wanaishi<br><br>Endelevu | Kamati ya Uratibu wa Mradi<br><br>Mabaraza ya Vijiji,<br><br>Kamati ya Ujenzi wa Shule |

| Na. | Masuala | Athari zinazoweza kutokea | Njia za Kupunguza Madhara | Muda | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | • Kutumia lugha za asili katika vikao kwa kutumia wakalimani pale inapohitajika.<br>• Kutoa taarifa mbalimbali kwa kutumia lugha za asili na sio kutumia Kiswahili pekee.<br>• Kuhakikisha kwamba makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi yanashirikishwa katika majadiliano hasa pale ambapo makundi haya yana nafasi ndogo au hayana nafasi kabisa ya kushirikishwa kwenye mabaraza ya vijiji. | | |

**Mpango wa Makundi ya Watu Walio katika Mazingira Hatarishi**

Mpango wa Makundi ya Watu Walio katika Mazingira hatarishi utaandaliwa kupitia ushirikishwaji, na unaweza kubadilika kulingana na hali halisi kwa kutumia mbinu shirikishi. Utekelezaji wa mpango wa makundi ya watu walio kwenye mazingira hatarishi katika mradi utajenga mazingira ya kuboresha hali na ustawi wa maisha yao. Mipango yote ya makundi ya watu walio kwenye mazingira hatarishi itakuwa na maeneo yafuatayo:

1. Muhtasari wa muundo wa kisheria na kitaasisi wa makundi ya watu walio kwenye mazingira hatarishi.
2. Taarifa za awali za idadi ya watu, kijamii, kitamaduni, ardhi wanayomiliki (iwe kwa njia za kienyeji au kwa hati miliki na mipaka yake) na rasilimali wanazotegemea kujikimu kimaisha.
3. Muhtasari wa tathmini ya jamii ambao utatoa mchanganuo wa uwezo wa kijamii na kiuchumi, muktadha wa kimazingira kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.
4. Muhtasari wa majadiliano na makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi yaliyofanywa wakati wa maandalizi ya mradi.
5. Muundo wa kuhakikisha majadiliano huru yanafanyika na makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kabla na wakati wa maandalizi ya miradi na utekelezaji wake pamoja na ushahidi wa majadiliano kama yamefanyika.
6. Mpango kazi wa kuhakikisha makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi yanapata manufaa kwa mujibu wa utamaduni wao na pale itakapolazimika kujenga uwezo wa watekelezaji wa mradi.
7. Baada ya kubainisha athari zinazoweza kutokea kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi, mpango kazi utaandaliwa ili kuzuia, kupunguza, kurekebisha au kufidia athari hizo kulingana na taarifa zilizoainishwa katika mwongozo wa usimamizi wa masuala ya kijamii na mazingira.
8. Makadirio ya gharama na mpango wa malipo kwa makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi vitaandaliwa na mradi husika ambao pamoja na mambo mengine utawajibika kulipa gharama kwa jamii husika.
9. Utaratibu unaoeleweka wa mpango wa kupokea na kushughulikia malalamiko ya waathirika wanaotoka katika makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi kutokana na utekelezaji wa mradi uwekwe bayana. Wakati wa kuandaa utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko, Serikali itazingatia uwepo wa taratibu za kisheria na zile za kitamaduni za kutatua migogoro baina ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.
10. Utaratibu na viwango vinavyofaa vya usimamizi, tathimini, na utaoji wa taarifa za utekelezaji wa mpango kazi uliowekwa kuhusu makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi. Utaratibu wa usimamizi na tathimini ni lazima uzingatie majadiliano na makubaliano huru ya waathirika kutoka makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaanzisha utaratibu wa usimamizi kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI ambao ndio watekelezaji wa mradi ili kuhakikisha uandaaji na utekelezaji katika ngazi ya jamii wa mpango kazi wa kusaidia makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi. Utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko unatoa nafasi kwa wanajamii kutoa malalamiko yao na hivyo kuboresha utendaji na uwajibikaji.

Utekelezaji wa mikakati ya makundi ya watu walio katika mazingira hatarishi, utategemea idadi ya makundi hayo, mahali yanapopatikana na aina na ukubwa wa athari husika.

**Uwasilishaji wa Maoni Kuhusu Rasimu ya Mwongozo wa Makundi ya Watu Walio kwenye Mazingira Hatarishi**

Maoni kuhusu rasimu yanaweza kutolewa kwa kupitia njia zifuatazo:

**Vikao:**

| **Mkoa** | **Halmashauri** | **Ukumbi** | **Tarehe** |
|---|---|---|---|
| Singida | Singida Manispaa | Halmashauri | 08 November 2019 |
| Manyara | Babati Mji | Halmashauri | 11 November 2019 |
| Manyara (VG) | Mbulu Vijijini | Yaeda chini | 12 November 2019 |
| Pwani | Kibaha Mji | Halmashauri | 13 November 2019 |

**ANDIKO ZIMA LINAPATIKANA KUPITIA:**

**Tovuti**: www.moe.go.tz , www.tamisemi.go.tz

**Kwa Mawasiliano na Maoni:**

**Simu**: + 255 (26) 232 1 234, +255 26 296 3533

**Barua Pepe**: tabitha.etutu@moe.go.tz, tulinagwe.ngonile@tamisemi